



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



TANGAZO KWA WANANCHI WOTE

Tarehe 15/10/2024

1. Shule ya Sekondari Nyabichune imepokea fedha kwa ajili ya mradi wa **Ujenzi wa Nyumba Pacha Ya Watumishi** fedha kutoka Mpango wa CSR.
2. Mkuu wa Shule Ya Sekondari Nyabichune anawatangazia mafundi wote wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya ufundi walete maombi ya ufundi kwa kazi zifuatazo:

**Ujenzi wa Nyumba Pacha
ya Mtumishi**

LGA/067/2024/2025/W/UJ/NYBSS/01

SIFA ZA MAFUNDI

- Mwombaji awe Mtanzania (awe na kitambulisho cha taifa/mpiga Kula)
- Awe na barua ya utambulisho kutoka kwa mwenyekiti wa mtaa au **Mtendaji wa Kijiji** ikiwa na picha.
- Mwombaji awe na akaunti Benki
- Mwombaji awe tayari kukosolewa au kushauriwa na mhandisi wa ujenzi
- Mwombaji asiwe amewahi kushitakiwa kwa kosa lolote la kihalifu au kushindwa kutekeleza kazi zinazofanana na hizi.
- Mwombaji awe na uwezo wa kusoma michoro na ramani na kutafasiri (local fundi)
- Mwombaji awe na uzoefu wa kujenga majengo yalioorodheshwa hapo hapo juu
- Fundi atakayefaulu kupata kazi atapewa jaribio la kujenga kwa vitendo.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. Nyaraka zote zinapatikana katika ofisi ya Mkuu wa Shule Ya Sekondari Nyabichune bure, iliyopo kijiji Cha Nyabichune **Kata ya Matongo Halmashauri ya Wialaya ya Tarime.** kuanzia saa **2:00 Asubuhi** hadi saa **9:30 Alasiri Siku za kazi. (Jumatatu hadi Ijumaa).**
2. Maombi yote yawekwe kwenye bahasha na kufungwa vizuri na kuandikwa juu ya bahasha maneno ya fuatayo:-
Mkuu Wa Shule,
Shule Ya Sekondari Nyabichune,
S.L.P 93,
Tarime.

MFANO

Ujenzi wa Nyumba Pacha ya Watumishi
Zabuni Na LGA/067/2024/ 2025/W/UJ/NYBSS/01

3. Mwisho wa kurudisha maombi ni tarehe **21/10/2024** saa **4:00 Asubuhi** na **baadaye zitafunguliwa saa 4:30 asubuhi.** Maombi/zabuni zitakazochelewa, za kielektroniki, na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji wa zabuni kwa hali yoyote ile hazitapokelewa wala hazitakubaliwa kwa tathimini.



Innocent J. Munishi
Mkuu wa Shule
Shule ya Sekondari Nyabichune
Tarime